

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MKATABA WA KUUZIANA SHAMBA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 06 Mwezi OKTOBA 2020
KATI YA

IBRAHIM A. LWELENJA, WA S.L.P 1139, NYAMKAZI, BUKOBA ambaye katika mkataba huu atajulikana kama muuzaji pamoja na warithi wake kwa upande mmoja.

NA

SUPREME PERCH LTD WA S.L.P 173, MWANZA, ambaye katika mkataba huu atafahamika kama MNUNUZI kwa upande mwingine pamoja na warithi wake.

KWA KUWA muuzaji ni mtanzania na amehiari kuuza shamba lake kwa Mnunuzi kwa gharama na masharti yaliyotajwa kwenye mkataba huu.


NA KWA kuwa MNUNUZI amekubali kununua shamba hili kwa gharama na masharti ya mkataba huu baada ya kujiridhisha kuwa ni mali ya muuzaji.


HIVYO BASI, Mkataba huu unaweka masharti vafuatayo:-

1. Kwamba gharama ya kuuza na kununua shamba hili ni **shilingi milioni ishirini na tisa za kitanzania** na mnunuzi amelipa pesa zote taslimu kwa tarehe na siku ya kusaini mkataba huu.
2. Kwamba, shamba halijapimwa na lipo maeneo ya Lubambangwe, Chato mkoa Geita, lina vipimo vya Hekari 14.8 na majirani ni Supreme Perch kwa upande wa Mashariki, Simoni Makoye Mayeka kwa upande wa Magharibi, Kaskazini na Kusini.
3. Kwamba, mnunuzi amejiridhisha kuwa shamba halina mgogoro wowote na hivyo amelipa pesa taslimu kulingana na mkataba huu na muuzaji hadai chochote kwenye shamba hili.
4. Kwamba, tangu tarehe ya kusaini mkataba huu umiliki umehama rasmi kutoka kwa muuzaji kwenda kwa mnunuzi na muuzaji hatadai chochote kwenye shamba hili na wala kuingia yeye mwenyewe au wakala wake.
5. Kwamba, ikiwa utatokea mgogoro wowote kuhusu umiliki sheria za Tanzania zitatawala.

Mkataba huu umesainiwa na kushuhudiwa kama inavyooneshwa hapa chini.


UMESAINIWA hapa **BUKOBA** na **IBRAHIM A. LWELENJA**
ambaye ametambulishwa kwangu
na **PETEUS MUYALINGWA** ambaye namfahamu binafsi
mbele yangu leo tarehe 06 mwezi OKTOBA, 2020


06/10/20
MUUZAJI

Saini 
Jina EVANCE KAIZA JULIDE
Anwani S.L.P 1245, BUKOBA
Wadhifa WAKILI



UMESAINIWA hapa BUKOBA
na kuwekwa MHURI na SUPREME PERCH LTD
mbele yetu leo tarehe 06 mwezi OKTOBA 2020



Saini _____
Jina ~~Mwandishi Mwanj Aluripia~~
Anwani 1120, BUKOBA
Wadhifa: ~~VENTURA MWAJIBER~~

Saini _____
Jina Hamza Mustafa Ismail
Anwani S.L.P 173 Mwanza
Wadhifa: Quality Assurance Manager.

Umecndaliwa na:

Pereus Mutasingwa Sarapion

Advocate, Notary Public and Commissioner for Oaths

P.O Box 1620, Bukoba.

Cell: 0758357858

Email: pereussarapion@gmail.com

